TANGAZO LA SERIKALI NAMBA.189 la tarehe 17/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA MAPINDUZI 'A' NA 'B' YA MWAKA 2023.

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la. Mapinduzi 'A' na 'B' ya Mwaka 2023.

Kutangaza Eneo la upangaji
Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (Mpango wa Urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Kuandaa na kuhifadhi Mipangokina

3. Mipangokina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na
kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M1 yenye majira - nukta 431443MS, 8791533KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa kufuata barabara ya Tunduru - Masasi mpaka kwenye makutano na barabara ya Mangaka- Mtambaaswala kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M2 yenye majira - nukta 432579MS, 8791584KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa kufuata barabara ya Mangaka - Mtambaswala kwa umbali wa kilomita 0.73 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M3 yenye majira - nukta 432493MS, 8790861KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa $66^0$ 05'42'' kwa umbali wa kilomita 0.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M4 yenye majira - nukta 432298, 8790945; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa $12^0$ 14'51'' kwa umbali wa kilomita 0.22 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M5 yenye majira - nukta 432344MS, 8791163KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa $87^0$ 15'52'' kwa umbali wa kilomita 0.15 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M6 yenye majira - nukta 432190MS, 8791170KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa $70^0$ 30'04'' kwa umbali wa kilomita 0.17 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M7 yenye majira - nukta 432031MS, 8791113KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa $88^0$ 32'03''kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi mto Lidede kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba M8 yenye majira - nukta 431491MS, 8791097KZ;baada ya hapa mpaka unaelekea Kaskazini kwa kufuata mto Lidede hadi ulipoanzia."

Dodoma
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi*